SUMAIT University Journal (SUJ)
eissn (2953-2698)
Issue No.18 June 2026

Ulinganishi wa Mtindo Unaojitokeza Baina ya Kasida na Nashidi za Kiswahili Zanzibar.

Baraka Salum Mataimba
barakasulumu@gmail.com
Department, Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni
Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)

Hassan Gora Haji
hassan.haji@suza.ac.tz
[1 2]*Department, Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni*
Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)

Received: Januray: 2026, Accepted: Abirl 20226, published: June 2026
© SUMAIT University Journal 2026

Abstract
This article compares stylistic between kasida and nashidi in Kiswahili literature within the Zanzibar community. The study is motivated by the prominence of these genres in religious and social contexts. The main objective is to identify shared stylistic features between the two forms. Data were collected through document analysis and interviews with composers and performers of kasida and nashidi. A descriptive approach was used in analyzing the data. The study is guided by Structuralism Theory, which emphasizes the analysis of linguistic and structural elements in literary works. Findings reveal that kasida and nashidi share several stylistic features such as repetition, poetic language, figurative expressions, use of grammatical persons, as well as proverbs and symbolism. The study concludes that the two genres are closely related in their artistic use of language in Kiswahili literature.

Keywords: Kasida, Nashidi, Style, Structuralism, Swahili Literatur

Ikisiri
Makala hii inalinganisha mfanano wa mtindo unaojitokeza baina ya kasida na nashidi za Kiswahili katika jamii ya Zanzibar. Utafiti huu umechochewa na ukweli kwamba kasida na nashidi ni tanzu za fasihi ya Kiswahili zinazotumika sana katika matukio ya kidini na kijamii. Lengo kuu ni kubainisha vipengele vya kimtindo vinavyofanana katika tanzu hizi mbili. Data zilikusanywa kwa kutumia uchambuzi wa nyaraka na usaili. Uchambuzi umefanywa kwa mkabala wa kimaelezo na umeongozwa na Nadharia ya Umuundo. Matokeo yanaonesha kuwa kasida na nashidi zinafanana

katika matumizi ya takriri, lugha ya kishairi, tamathali za semi, nafsi mbalimbali, mafumbo na methali. Utafiti unahitimisha kuwa kuna uhusiano mkubwa wa kimtindo baina ya tanzu hizi.

1.0 Utangulizi

Fasihi ya Kiswahili ni miongoni mwa nyenzo muhimu zinazotumika katika kuhifadhi, kuendeleza na kuwasilisha utamaduni, historia, maadili pamoja na mitazamo ya jamii za Waswahili. Fasihi hii imeendelea kukua kwa kupitia tanzu zake mbalimbali kama vile ushairi, tamthilia, riwaya, hadithi na fasihi simulizi. Ndani ya mazingira ya jamii za Kiislamu za Afrika Mashariki, hususan Zanzibar, kasida na nashidi zimeendelea kuwa sehemu muhimu ya maisha ya kijamii, kidini na kiutamaduni. Tanzu hizi zimekuwa zikitumika kama nyenzo za kufundishia maadili, kuhamasisha mshikamano wa kijamii, kueneza mafundisho ya dini ya Kiislamu pamoja na kuburudisha jamii katika matukio mbalimbali ya kijamii na kidini.

Kwa mujibu wa [1], fasihi ya Kiswahili huakisi maisha halisi ya jamii kwa kutumia lugha yenye mvuto wa kisanaa inayobeba mafunzo, maadili na falsafa ya jamii husika. Katika muktadha huo, kasida na nashidi zimeendelea kudhihirisha namna lugha ya Kiswahili inavyoweza kutumika kisanaa katika kuwasilisha maudhui yenye uzito wa kijamii na kidini. Zanzibar ikiwa ni moja ya kitovu muhimu cha ustaarabu wa Waswahili na dini ya Kiislamu Afrika Mashariki, imekuwa na mchango mkubwa katika ukuzaji na uenezaji wa tanzu hizi za kifasihi.

Kasida ni utungo wa kishairi wenye asili ya Kiarabu ambao umeathiriwa kwa kiasi kikubwa na utamaduni wa Kiislamu. Tanzu hii hutumika zaidi katika kusifu Mtume Muhammad (S.A.W), kuelezea mafundisho ya dini pamoja na kuhimiza maadili mema katika jamii. Kwa upande mwingine, nashidi ni nyimbo au tungo za kidini zinazowasilishwa kwa njia ya uimbaji wa kishairi na mara nyingi huwasilisha ujumbe wa kiroho, maadili na mafunzo ya kijamii. Kwa mujibu wa [3], fasihi simulizi ya Kiafrika hujengwa katika utendaji wake kwa kutumia mbinu za kifani zinazohusisha urari wa lugha, uradidi wa sauti pamoja na matumizi ya lugha ya picha ili kuleta mvuto kwa hadhira. Maelezo hayo yanaonesha kuwa kasida na nashidi hushirikiana katika matumizi ya mbinu mbalimbali za kisanaa zinazochangia ubora wa kazi hizo.

Katika jamii ya Zanzibar, kasida na nashidi hutumika katika mazingira mbalimbali kama vile maulidi, madrasa, harusi, baraza za dini, shughuli za kijamii na matamasha ya kiislamu. Tanzu hizi zimekuwa zikivutia hadhira kutokana na matumizi ya lugha ya kishairi yenye mvuto, matumizi ya tamathali za semi, urari wa vina na mizani pamoja na mbinu za kisanaa zinazosaidia kufikisha ujumbe kwa ufasaha. [2] anaeleza kuwa mtindo ni jumla ya mbinu na taratibu zinazotumiwa na msanii katika kuwasilisha kazi yake ya kifasihi. Aidha [4], wanafafanua kuwa mtindo hujitokeza kupitia namna lugha inavyotumiwa kisanaa ili kuibua athari maalumu kwa hadhira. Hivyo basi, uchambuzi wa mtindo husaidia kuelewa namna msanii anavyotumia vipengele vya lugha katika kuwasilisha dhamira na maudhui yake.

Pamoja na kuwepo kwa tafiti mbalimbali kuhusu ushairi wa Kiswahili, bado kuna upungufu wa tafiti zinazochunguza kwa kina mfanano wa kimtindo kati ya kasida na nashidi katika mazingira ya Zanzibar. Tafiti nyingi zimejikita zaidi katika maudhui, nafasi ya dini au historia ya tanzu hizi bila kuangazia kwa kina vipengele vya mtindo vinavyofanana baina yake. Hivyo basi, makala hii

inalenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza mfanano wa mtindo unaojitokeza baina ya kasida na nashidi za Kiswahili katika jamii ya Zanzibar.

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Umuundo ambayo hujikita katika kuchunguza miundo na matumizi ya lugha katika kazi za fasihi. Kwa mujibu wa Saussure kama alivyonukuliwa na [8], maana katika lugha hupatikana kupitia uhusiano wa vipengele mbalimbali vya lugha katika mfumo mzima wa kimawasiliano. Kwa msingi huo, nadharia hii imeonekana kuwa muafaka katika kuchunguza namna vipengele vya lugha kama vile takriri, tamathali za semi, matumizi ya nafsi, vina, mizani, methali na mafumbo vinavyojitokeza na kufanana katika kasida na nashidi za Kiswahili Zanzibar.

Kwa kuzingatia maelezo hayo, makala hii inalenga kuchambua mfanano wa mtindo unaojitokeza baina ya kasida na nashidi za Kiswahili Zanzibar kwa kuhusisha matumizi ya vipengele mbalimbali vya kiisimu na kifasihi vinavyotumika katika tanzu hizo mbili. Uchambuzi huu unatarajiwa kuongeza maarifa katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili na kutoa mchango katika tafiti za fasihi linganishi na elimu mtindo.

2.0 Kiunzi cha Nadharia ya Utafiti

Nadharia ni kauli au kanuni za jumla zinazotegemewa katika kuelezea au kuchambua jambo fulani. Kwa ujumla, nadharia ni mfumo wa mawazo unaotumiwa kuelezea na kuchambua masuala mbalimbali ya kisayansi au kijamii.

Utafiti huu umetumia Nadharia ya Umuundo katika kulinganisha na kufananisha mitindo ya kasida na nashidi. Hivyo basi, utafiti huu utaongozwa na Nadharia ya Umuundo katika uwanda wa fasihi linganishi.

2.1 Nadharia ya Umuundo katika Fasihi Linganishi

Nadharia ya Umuundo ni nadharia ya uhakiki wa kazi za fasihi inayochunguza kaida na muundo wa kazi ya fasihi. Kwa mujibu wa [2], nadharia hii inaweka mkazo mkubwa katika muundo wa kazi ya fasihi badala ya kumzingatia mwandishi wake.

[4] wanaeleza kuwa nadharia hii ina uhusiano mkubwa na elimu mtindo kwa sababu inachambua matumizi ya lugha katika kazi za fasihi. Hii ina maana kuwa Nadharia ya Umuundo inajikita moja kwa moja katika uchambuzi wa mtindo katika kazi za fasihi.

[7] anaeleza kuwa elimu mtindo inahusisha uchambuzi wa vipengele vya kiisimu kama vile fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki katika kazi za fasihi. Vipengele hivyo hutumika kubainisha na kuchambua namna lugha ilivyotumika katika kazi mbalimbali za fasihi.

Kwa upande mwingine, [8] wanaeleza kuwa Nadharia ya Umuundo hujikita katika uchambuzi wa matawi ya isimu ya lugha kama vile fonetiki, fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki na jinsi vipengele hivyo vinavyotumiwa katika kazi za fasihi.

Kwa ujumla, maelezo hayo yanaonesha kuwa Nadharia ya Umuundo inalenga kuchambua vipengele vya lugha na muundo wa kazi ya fasihi ili kubainisha mtindo uliotumiwa na msanii.

Nadharia ya Umuundo ni miongoni mwa nadharia kongwe katika uchambuzi wa kazi za fasihi. Baadhi ya waasisi wa nadharia hii ni pamoja na mwanaisimu wa Uswisi Ferdinand de Saussure,

pamoja na Claude Levi-Strauss na Roland Barthes. Wataalamu hawa walisisitiza umuhimu wa kuchunguza muundo wa lugha katika kuelewa kazi za fasihi.

2.2 Misingi Mikuu ya Nadharia ya Umuundo

Katika utafiti huu, Nadharia ya Umuundo imetumika kupitia misingi ifuatayo:
i. Vipengele vya lugha hujenga mfanano au utofauti wa kazi za fasihi.
Kwa mujibu wa nadharia hii, kufanana au kutofautiana kwa kazi za fasihi hutegemea namna vipengele vya lugha vinavyotumiwa katika kazi hizo. Vipengele hivyo vinaweza kuwa vina, mizani na takriri katika ushairi ambavyo ni vipengele vya kifonolojia katika isimu. Aidha, uradidi wa maneno unaweza kuangaliwa kama kipengele cha kimofolojia, wakati mitindo ya mishororo na kibwagizo inaweza kuhusishwa na sintaksia.
ii. Maana na athari za lugha hutokana na uhusiano wa vipengele vya lugha.
Kwa mujibu wa nadharia hii, maana katika kazi ya fasihi hutokana na uhusiano uliopo kati ya vipengele mbalimbali vya lugha kama vile fonolojia, mofolojia na sintaksia. Uhusiano huo huweza kuleta athari za kisemantiki na kimtindo katika kazi ya fasihi.
iii. Muundo wa kazi ya fasihi ni muhimu katika uchambuzi wa kazi za fasihi.
Nadharia ya Umuundo inaeleza kuwa uchambuzi wa kazi ya fasihi unapaswa kuzingatia zaidi muundo wa kazi hiyo pamoja na kanuni za utanzu husika.
Kwa msingi huo, nadharia hii imekuwa muafaka katika utafiti huu kwa sababu imewezesha kuchambua na kulinganisha mtindo wa kasida na nashidi katika jamii ya Zanzibar.

3.0 Mbinu ya Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data ndio hatua muhimu katika utafiti wa kisayansi. [5] anafafanua dhana ya ukusanyaji wa data kama zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha katika madhumuni yake ya utafiti. Aidha, [5] anasisitiza kuwa hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ah atua hii ya ukusanyaji wa data. Katika utafiti huu, data zimekusanywa kwa kutumia njia ya usaili, ushuhudiaji na udurusu matini.

3.1 Mbinu ya Usaili

[6], anaeleza kuwa usaili ni njia ya kukusanya taarifa ambayo inahusisha mazungumzo baina ya mtafiti na watafitiwa wake kuhusu mambo ambayo mtafiti anataka kuyafahamu. Majilio ya teknolojia yamewezesha kupanua ufanyikaji wa usaili. Kwa hiyo, si lazima mtafiti aonane ana kwa ana na mtafitiwa wake, bali huweza kutumia nyenzo za simu au kompyuta kuendesha usaili kupitia kupiga simu ya moja kwa moja, au kutumia mazungumzo kwa njia ya video kupitia mitandao ya kijamii kama vile WhatsApp, Skype au Telegram. Njia hii ilitumika ili kupata maelezo ya ziada kutoka kwa watafitiwa. Mtafiti alitumia maswali ya wazi ili kumuwezesha kuuliza maswali ya ziada pale ilipohitajika. Njia hii ilitumika kuhoji sampuli ya waghaniaji wa kasida, waghaniaji wa nashidi pamoja na wachambuzi wa kazi za fasihi. Kutokana na hali hiyo, utafiti huu ulitumia njia ya mahojiano ya ana kwa ana ili kupata fursa ya kupata maelezo ya zaidi kutoka kwa watafitiwa.

3.2 Mbinu ya Udurusu Matini

Wakati wa kukusanya data kutoka kwenye maandiko hayo mtafiti alisoma kwa umakini mkubwa neno, kirai na kila sentensi huku akiwa ananukuu data alizozikusudia ambazo zilijibu maswali ya utafiti wake. Hali hii ilitokana na maelezo ya [5] yanayoeleza kuwa udurusu matini unahitaji umakini mkubwa katika upitiaji wa matini kwa kuzingatia kila kitu katika matini hayo.

Mtafiti ametumia mbinu hii ili kuchunguza wataalamu wengine wamezungumzia vipi kasida ambayo ndio imeandikwa sana na kuzikusanya ili kupata mapitio ya maandiko na data zitakazoshadidi hoja za utafiti wetu.

3.3 Mbinu ya Ushuhudiaji

[6] anaeleza kuwa ushuhudiaji ni njia ya kukusanya taarifa ambapo mtafiti huwa katika eneo halisi la utafiti na kufuatilia jambo kwa karibu au ana kwa ana. Mtafiti amechaguwa mbinu hii kwa sababu kuna data zinazopaswa kukusanywa katika sehemu halisi. Mfano kuona jinsi nashidi na kasida zinavyo wasilishwa kwa hadhira yake. Mtafiti alilazimika kuhudhuria katika shughuli mbalimbali ambazo zilikuwa na ratiba ya kughaniwa kasida au nashidi au zote mbili. Mfano wa shughuli hizo ni pamoja na matamasha ya kasida na nashidi. Njia hii ilimsaidia mtafiti kukusanya data halisia na zenye ubora zaidi. Hivyo njia hii ni muhimu kwa ajili ya kupata data halisi.

4.0 Mfanano wa Mtindo katika Kasida na Nashidi

4.1 Takriri

[1] anaelezea kuwa takriri ni mbinu ya kisanaa inayotokana na kurudia maneno, silabi, au sentensi ili kuleta msisitizo au kuimarisha ujumbe fulani. Takriri, kwa maneno mengine, ni kitendo cha kurudia rudia kipengele cha lugha ili kuonesha umuhimu wa jambo fulani au hali inayotakiwa kusisitizwa. Mbinu hii inatambulika katika kazi za fasihi za Kiswahili, hususan katika kasida na nashidi, ambapo hutumika katika kurudia maneno, kiitikio, na sentensi. Kupitia nadharia ya linganishi, [7] anasisitiza kuwa fani ni msingi mkubwa unaoweza kuzalisha misingi midogo ya kisanaa, na takriri ni moja ya mifano ya mtindo unaojitokeza katika misingi hii. Mbinu ya takriri inaweza kuchambuliwa kwa vipengele mbalimbali, na kila kipengele kina mchango wake wa kipekee katika msisitizo na ubora wa kazi. Vipengele hivi ni pamoja na:

4.1.1 Takriri Silabi

Takriri ya silabi inahusisha kurudia sehemu ndogo ya neno, kama silabi moja au mbili, ili kuimarisha hisia au msisitizo. Katika kasida na nashidi za Kiswahili wasanii hutumia mtindo huu katika uandishi wao. Mfano Katika nashidi ya “Zinawiri Ndoa Zetu”;

*Zinawiri ndoa ze**tu**, Ya Rabi tunakuo**mba**,*
*Hatuwezi pekeye**tu**, bila ya wewe muu**mba**.*

Silabi “tu” na “mba” zimejirudia “tu” imejirudia katikati ya beti na “mba” imejirudia mwishoni mwa beti kuleta mvuto kwa msikilizaji. Mfano katika kasida ya “Subira Jambo la Kheri”;

*Subira jambo la khe**ri**, kiumbe ukiwa na**yo**,*
*Mola hukulipa khe**ri**, ukiishika kwa mo**yo**,*

Silabi “ri” na “yo” zimejirudia “ri” imejirudia katikati ya beti na “yo” imejirudia mwishoni mwa beti kuleta mvuto kwa msikilizaji.

Uchambuzi huu unadhirisha kuwa nashidi na kasida zimekuwa zinafanana katika kipengele hiki kutokana na fani zote hizi kuwa na mtindo sawa. Hali hii inatokana na msingi wa Nadharia ya Umuundo unaoeleza kuwa mfanano wa kazi ya moja ya kifasihi na nyengine unatokana na namna moja ya utumiaji wa kipengele cha kiisimu katika lugha iliyotumika. Jambo ambalo linaonesha kuwa kipengele cha kifonolojia kimetumika kwa namna sawa katika kasida na nashidi za Kiswahili katika jamii ya Zanzibar.

4.1.2 Takriri Neno

Takriri ya neno ni kurudia neno kamili ili kutoa msisitizo. Katika kasida na nashidi za Kiswahili wasanii hutumia mtindo huu katika uandishi wao. Katika nashidi ya “Asante”:

Pokea **asante**, Moyoni **asante**
Ukifike popote, Hubbi, **asante**
Vizuri ikamate, Kwa mahaba yote
Pokea **asante**Hubbi, **asante**
Asante asante

Kurudia neno “asante” kunasisitiza shukrani na thamani yake katika muktadha wa kijamii na kifasihi. Mfano katika kasida ya “Zamzam”;

Ya **Zamzama** Ya **Zamzama**
Alikunywa Tumwa Maji mema
Ya **Zamzama**

Katika kasida hii neno “Zamzama” limerudiwa rudiwa mara nyingi. kurudiwa rudiwa neno hilo ni kuonesha msisitizo kuhusu maji haya ya zamzam. Mbinu hii huonesha upekee wa mwandishi katika kubuni kazi ya fasihi.

Utafiti huu umebaini kuwa, nashidi na kasida zimekuwa zinafanana katika kipengele hiki kutokana na fani zote hizi kuwa na mtindo sawa. Hali hii inatokana na msingi wa Nadharia ya Umuundo unaoeleza kuwa mfanano wa kazi ya moja ya kifasihi na nyengine unatokana na namna moja ya utumiaji wa kipengele cha kiisimu katika lugha iliyotumika. Jambo ambalo linaonesha kuwa kipengele cha kimofolojia kimetumika kwa namna sawa katika kasida na nashidi za Kiswahili katika jamii ya Zanzibar.

4.1.3 Takriri Mshororo

Hii ni mbinu ya kurudia msemo mfupi au mstari mfupi kwa lengo la kuzidisha mvuto wa beti. Watunzi wa kasida na nashidi hutumia mtindo huu kwenye kazi zao. Mfano katika nashidi ya "Ushoga":

You see **Adam aliumbiwa Hawa wazungu humwita Eva**,
Slow down sijaeleweka **Adam aliumbiwa Hawa wazungu humwita Eva**.

Mshororo "Adam aliumbiwa Hawa wazungu humwita Eva" unarudiwa ili kuimarisha kuonesha msisitizo kuwa Mungu alimuumba mwanamke na mwanaume sio mwanaume na mwanaume hivyo watu waache mapenzi ya jinsia moja. Mfano wa kasida ya "Tushangilie Harusi"

Imetimia harusi njema tuloingojea,
Mola kaleta wepesi dada yetu kaolewa,
Imetimia harusi njema tuloingojea,
Mola kaleta wepesi kaka yetu ameoa,

Mshororo "imetimia harusi njema tuloingojea" umerudiwa mara mbili kwenye beti kuketa mvuto na kuonesha furaha ya kutimia harusi.
Uchambuzi huu unadhirisha kuwa nashidi na kasida zimekuwa zinafanana katika kipengele cha sintaksia katika isimu ya lugha ya Kiswahili. Jambo ambalo linaonesha kuwa fani zote hizi zimekuwa kuwa na mtindo sawa katika matumizi yake ya sintakisia. Hoja hii inatokana na msingi wa Nadharia ya Umuundo unaoeleza kuwa mfanano wa kazi ya moja ya kifasihi na nyengine unatokana na namna moja ya utumiaji wa kipengele cha kiisimu katika lugha iliyotumika. Hivyo ni wazi kuwa, nashidi zinafanana na kasida katika mtindo wa kutumia kipengele cha sintaksia.

4.1.4 Takriri Kiitikio

Hii ni takriri ya mstari unaojirudia katikati ya beti kadhaa. Ni mojawapo ya vipengele vinavyojitokeza sana katika kasida na nashidi. Mfano wa kiitikio tunaweza kuona katika kasida ya Subira "Jambo la Kheri";

Subira jambo la kheri
Kiumbe ukiwa nayo
Mola hukulipa kheri
Ukiishika kwa moyo x2

Katika kasida hii kiitikio kilianza na kilisomwa kila baada ya beti. Kwa upande wa nashidi marudio ya kiitikio tunaweza kuyaona katika iitwayo ASANTE;

Pokea asante, Moyoni asante
Ukifike popote, Hubbi, asante
Vizuri ikamate, Kwa mahaba yote
Pokea asanteHubbi, asante
Asante x2

Katika nashidi hii kiitikio kilisomwa mwanzo na kila baada ya beti. Kiitikio huchangia msisitizo, mvuto wa kiasili, na urahisi wa kumbukumbu kwa wasikilizaji.

Kutokana na uchambuzi huo, utafiti umebaini kuwa nashidi na kasida zinafanana katika mtindo wa kutumia kipengele cha sintaksia katika isimu ya lugha ya Kiswahili. Jambo ambalo linaonesha kuwa fani zote hizi zimekuwa na mtindo sawa katika matumizi yake ya sintakisia. Hoja hii inatokana na msingi wa Nadharia ya Umuundo unaoeleza kuwa mfanano wa kazi ya moja ya kifasihi na nyengine unatokana na namna moja ya utumiaji wa kipengele cha kiisimu katika lugha iliyotumika. Hivyo ni wazi kuwa, nashidi zinafanana na kasida katika mtindo wa kutumia kipengele cha sintaksia.

4.1.5 Takriri Kirai

Takriri kirai inahusisha kurudia kirai au kifungu kinachounda mpangilio wa kishairi katika beti. Katika kasida na nashidi za Kiswahili huweza kurudia vifungu vya maneno katika ubeti. Mfano katika nashidi ya "Wali harage";

..... tunataka kupokea ila tunahofia
Shibe isije ingia na ndani kuna ***wali harage***
Wali harage *aah aah wali harage aah* ***wali harage***

Katika nashidi hii kirai cha "wali harage" kimerudiwa mara nyingi kuonesha msisitizo kuwa wali harage ni mtamu sana na watoto wanaupenda. mfano katika kasida ya "Zamzam";

Ya Zamzama Ya Zamzama
Alikunywa chumwa Maji mema
Ya Zamzama

Katika kasida hii kirai cha "Ya Zamzama" kimerudiwa rudiwa mara nyingi. kurudiwa rudiwa kirai hicho ni kuonesha msisitizo kuhusu maji haya ya zamzam. Takriri ni mtindo muhimu unaojitokeza kwa nguvu katika kasida na nashidi za Kiswahili Zanzibar. Kurudia kwa sauti, silabi, neno, mshororo, ubeti, kiitikio, na kirai kunachangia msisitizo, mvuto wa kisanaa, na uhalisia wa ujumbe wa kifasihi. Hoja hii inatokana na msingi wa Nadharia ya Umuundo unaoeleza kuwa mfanano wa kazi ya moja ya kifasihi na nyengine unatokana na namna moja ya utumiaji wa kipengele cha kiisimu katika lugha iliyotumika. Hivyo ni wazi kuwa, nashidi zinafanana na kasida katika mtindo wa kutumia kipengele cha sintaksia.

4.2. Uwasilishaji wa Mtu Mmoja au Kikundi wakati wa uimbaji

Katika kasida na nashidi huweza kusomwa na mtu mmoja au kikundi cha watu. [3] anafafanuwa kuwa uwasilishaji wa fasihi simulizi unaweza kufanywa na mtu mmoja, mwimbaji, msimulizi au mshairi pia uhusisha ushirikiano wa kundi. Watoa taarifa wameweza kuelezea kuwa usomaji wa kasida wa mtu mmoja na kundi ni mtindo ambao kila mmoja hufanyika kwa lengo mahsusi na unaladha yake, lengo la kusoma mtu mmoja ni kufikisha ujumbe unao muhusu yeye zaidi na mara nyingi usomaji wa kundi huwa na lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii. Mfano wa kasida iliyosomwa na mtu mmoja peke yake ni ile ya "Mtume Wetu Hashimu";

Mtume wetu hashimu
Alikuwa muadhamu
Mbele ya mola karimu
Kuliko kila nabiya
(Kakamilika namna
Mfano wake hakuna) ×2

Kasida iliyosomwa na kikundi cha watu ni kasida ya “Akayumbayumba Ngamia” iliyoimbwa na wanafunzi watatu wa Al-madrasatul Nasrul Islamia;

Wasomaji wote kwa pamoja
Akayumba yumba ngamia kwenda Madina
Huku akilia machozi yamfaraji x2

Msomaji wa kwanza
Wakubwa wa Maka
Walifadhaika

Msomaji wa pili
Waliposhituka
Tumwa ametoka

Kasida hii inamuelezea Mtume Muhammad (s.a.w) alivyotoka Makka kwenda Madina wasomaji watatu walishiriki kusoma kiitikio na wawili kusoma ubeti. Kwa upande wa nashidi iliyowasilishwa na mtu mmoja pekee ni nashidi iitwayo “Wasia”

Mwanangu ooh mwanangu
Kipenzi cha moyo wangu
Sogea karibu yangu
Nikupe wasia wangu

Kwa upande wa nashidi iliyoimbwa na zaidi ya mtu mmoja ni nashidi ya “UNAYO SIRI”, iliyosomwa na watu wawili;

Msomaji wa kwanza
Je una siri Abdallah?
Baina yako na Allah
Je na sadaka ya lillah
Aijua yeye Allah

Msomaji wa pili
Utaporudi kwa Allah
Ikuepushe ‘adhabaallah
Uingie pepo ya Allah
Useme Alhamdulillah

Wasomaji wote kwa pamoja
Je una siri Abdallah?
Baina yako na Allah
Je na sadaka ya lillah
Aijua yeye Allah
Utaporudi kwa Allah
Ikuepushe 'adhaba Allah
Uingie pepo ya Allah
Useme Alhamdulillah

Kwa hivyo, kupitia nashidi na kasida zilizotangulia tumeona namna waimbaji wa kasida na nashidi wanavyoziwasilisha kazi hizo akiwa mtu mmoja pekee au kikundi cha watu. Mitindo yote miwili huweza kutumika kwa lengo mahsusi. Matokeo haya yanathibitika kupitia msingi wa Nadharia ya Umuundo unaoeleza kuwa, tafauti za kazi moja ya fasihi na nyingine inatokana na namna kazi hizo zinavyotumia sifa na vipengele vya lugha na fasihi yenyewe. Hivyo, kutafautiana katika sifa hii, kunadhihirisha tafauti ya kasida na nashidi katika muktadha huu.

4.3 Utunzi wa Kishairi

Utunzi ni usanifu au utungaji [13]. [2] anaelezea shairi ni neno linaloelezea utungo wenye muundo maalamu katika mpangilio wa maneno, utumiaji wa lugha ya mkato na unaelezea suala fulani. Utunzi wa kishairi ni kitendo cha kuunda au kuandika kwa kufuata arudhi za kishairi kama vile beti, mizani, mishororo, vina nakadhalika.

Nashidi na kasida, zote mbili hutungwa na kuandikwa kwa kufuata arudhi za kishairi, watoa taarifa wameweza kuelezea kuwa kasida na nashidi za Kiswahili huchunga kanuni za utunzi wa kishairi kwa kuleta mvuto kwa wasikilizaji. Hivyo kasida na nashidi hutumia arudhi za kishairi kama vile beti kasida na nashidi fani hizi zote huwa na beti. [9] anaelezea kuwa beti ni kifungu cha mistari ya kishairi kinachofanya kazi ya kimuundo na kimaudhui ndani ya shairi. Mfano wa beti katika kasida ya "Ubinafsi"

Dhamiri aliiweka na ahadi kutoa
Atawafanyisha wengi bila kujua
Wajione bora mabega kutanua
Wakifanya wao sawa wengine balaa

Kasida hii ina beti yenye mistari minne. Mfano wa beti katika nashidi ya "Mrembo Elena"

Alilelewa malezi mema
Akaishi na kubwa heshima
Tena alikuwa kashikamana na dini njema
Watu wakamwita jina lake mrembo Elena

Nashidi hii pia inamistari minne katika ubeti wake, pia katika kasida na nashidi hutumia vina kwa kuleta mvuto katika usomaji wake. [2] anaelezea kuwa vina ni urudiaji wa sauti fulani katika mistari ya beti kwa lengo la kuimarisha mdundo, urari na usanii wa kishairi. Mfano wa vina katika kasida ya "Ubinafsi"

*Dhamiri aliiweka na ahadi kuto**a***
*Atawafanyisha wengi bila kuju**a***
*Wajione bora mabega kutanu**a***
*Wakifanya wao sawa wengine bala**a***

Kasida hii imetumia vina vya “a”. Mfano wa nashidi ya “Mrembo Elena”;

*Alilelewa malezi me**ma***
*Akaishi na kubwa heshi**ma***
*Tena alikuwa kashikamana na dini nje**ma***

Nashidi hii imetumia vina vya “ma”. Pia kuna baadhi ya nashidi hufuata urari wa vina na mizani. [10] anafafanua kuwa mizani ni idadi ya silabi zilizopo katika kila mstari wa beti ambazo hufuata kanuni za kishairi ilikuleta mpangilio wa kisanaa. Mfano wa kasida ya “Akayumbayumba Ngamia”

Wa – ku –bwa – wa – Ma –ka
1 2 3 4 5 6
Wa -li -fa -dha -i -ka
1 2 3 4 5 6
Wa - li - po - shi - tu -ka
1 2 3 4 5 6
Tu –mwa – a – me –to –ka
1 2 3 4 5 6

Kasida hii imetuia mizani sita katika kila mstari kwenye ubeti wake. Mfano wa nashidi ya “Wasia”

Mwa – na - ngu – o – h – mwa – na – ngu
1 2 3 4 5 6 7 8
Ki – pe - nzi – cha - mo – yo - wa – ngu
1 2 3 4 5 6 7 8
So – ge – a - ka – ri – bu – ya – ngu
1 2 3 4 5 6 7 8
Ni – ku – pe – wa – si – a – wa - ngu
1 2 3 4 5 6 7 8

Nashidi hii imetumia mizani nane katika kila mstari kwenye ubeti wake. Matokeo haya yanathibitika kupitia msingi wa Nadharia ya Umuundo unaoeleza kuwa, tafauti za kazi moja ya fasihi na nyingine inatokana na namna kazi hizo zinavyotumia sifa na vipengele vya lugha na fasihi yenyewe. Hivyo, kutafautiana katika sifa hii, kunadhihirisha tafauti ya kasida na nashidi katika muktadha huu.

4.4 Matumizi ya Nafsi

Matumizi ya nafsi katika fasihi yanahusu namna msanii anavyochagua kuwasilisha simulizi kwa kutumia nafsi ya kwanza, pili na tatu. Hii ni mbinu ya kifani inayosaidia kuwasilisha vyema maudhui, hisia na mtazamo wa kazi ya fasihi. [2] anaelezea kuwa nafsi ni mtazamo au sauti ya msimulizi inayotumika katika kazi ya fasihi kuonesha uhusiano kati msimulizi, wahusika na

hadhira. Matumizi ya nafsi ni mbinu nyengine inayotumiwa na watunzi wa kasida na nashidi, watoa taarifa wameelezaea kuwa nafsi hizi hutumika ili kupata urari wa vina na mizani au kuifanya kasida na nashidi ziweze kuwa katika hali zinazokubalika na kuwavutia wasomaji na wasikilizaji pia ni mbinu ambayo huonesha upekee wa msomaji. Mfano wa nafsi ni kama zifuatazo:

Nafsi ya kwanza umoja iliyotumika katika nashidi ya "Niacheni";

***Ni**liishi thamani sina, na nilikuwa shidani*
***Ni**kapata tabu sana, na nikawa tafarani*
***Ni**mazito yaliyonikuta, balaa na mitihani*
***Ni**kakosa hata pakushika, nikabakia shidani*

Katika nashidi hii matumizi ya nafsi ya kwanza umoja yametumika, msanii ameweza kuelezea maisha yake namna alivyopitia shida katika maisha yake pia neno "Niliishi" linaonesha wazi matumizi ya nafsi ya kwanza umoja kwa msanii kujiongelea, pia zipo kasida ambazo zimetumia nafsi ya kwanza umoja kama vile kasida ya "Ntakuona vipi" inayosema;

***N**takuona vipi ewe Tumwa wangu*
***Na**mizimezidi mnodhambi zangu*
Ooh nifanye nini ili niwe nawe Ashima

Kasida hii imetumia nafsi ya kwanza umoja ambapo msanii anajielezea kuwa anahofu ya kutokumwona Mtume Muhammad (s.a.w) kutokana na dhambi zake, neno "nifanye nini" linaonesha wazi matumizi ya nafsi ya kwanza umoja kwa msanii kujielezea mwenyewe.

Pia zipo nashidi ambazo zimetumia nafsi ya kwanza wingi kama vile nashidi inayoitwa "Ndoto Zetu" inayosema;

…. Usijali mwalimu tumekufahamu
Ndoto zetu sote nizamuhimu….

Nashidi hii imeweza kutumia nafsi ya kwanza wingi wanafunzi wanazungumza na mwalimu wao, wote kwapamoja wanatoa ahadi ya kufanya kazi nzuri neno "tumekufahamu" linaonesha wazi matumizi ya nafsi ya kwanza wingi. Pia zipo kasida zilizotumia nafsi ya kwanza wingi kama vile kasida ya "Tushikane";

***Tu**nawahasa wanashamsia tuungane sote kwa pamoja*
Umoja kitu azwima
Tafauti ziwe nyuma
Enyi nyote isilama tuungane kwa pamoya

Kasida hii imeweza kutumia nafsi ya kwanza wingi kwa kutumia maneno "tunawahasa", tuungane". Pia kasida ilo tumia nafsi ya pili umoja ni kasida ya "Harusi"

Ng'ari ng'ari anang'ara anameremeta bibi harusi
Anang'ara huyo huyo bibi harusi
Faghari kwa kweli cheleko cheleko mwana

Kasida hii imetumia nafsi ya pili umoja kwa kumsifu bi harusi, “anameremeta” linaonesha wazi matumizi ya nafsi ya pili umoja. Mfano wa nashidi iliyotumia nafsi ya pili umoja ni nashidi iitwayo “Ibrahim” kama ifuatayo;

IBRAHIM
Alizaliwa familia ya umasikini sana,
Ilifika wakati wasile, wazazi ili ashibe mwana....

Nashidi hii imetumia nafsi ya pili umoja kwa kuelezea maisha ya Ibrahimu neno “alizaliwa” linaonesha bayana atumizi ya nafsi y tatu wingi kwa msanii kumuelezea mtu mwingine. Mfano wa nashidi inayo tumia nafsi ya pili wingi ni nashidi inayoitwa “Hisani za Wapemba”

Hisani zenu zimenifanya kwamba
Nsiishe hamu kutembea Pemba
Huruka zenu zinawapamba

Nashidi hii imetumia nafsi ya tatu kwa kuwasifia Wapemba kwa uungwana wao kwa watu jambo ambalo limemvutia msanii, neno “zenu” linaonesha wazi matumizi ya nafsi ya pili wingi. Mfano wa kasida iliyotumia nafsi ya pili wingi inaitwa “Vazi jema”;

***M**kafanye jitihada upendo uimarike*
***Mu**himizane ibada ya kheri muyazidishe*
***Mu**kafurahie raha raha*
Ndoa yenu nyie raha raha
Umoja ni ngome hili nawaambia

Kasida hii imetumia nafsi ya pili wingi kwa kuwapa nasaha walofunga ndoa neno “mkafanye” linaonesha wazi matumizi ya nafsi ya pili wingi. Mfano wanashidi iliyotumia nafsi ya tatu umoja ni “Utukufu wa Allah”;

Bismillah Rrahmani Rrahim
Kuhimidiwa ni kwake Allah

Nashidi hii imetumia nafsi ya tatu umoja kwa kumuelezea Mwenyezi Mungu na utukufu wake neno “kwake” linaonesha wazi matumizi ya nafsi ya tatu umoja. Mfano wa kasida ilotumia nafsi ya tatu umoja ni kasida ya “Mtume Wetu Hashimu”;

Mtume wetu Hashimu
Alikuwa muadhwamu
Mbele ya Mola Karimu

Kasida hii imetumia nafsi ya tatu umoja kwa kumuelezea Mtume Muhammad (s.a.w), neno “alikuwa” linaonesha wazi matumizi na nafsi ya tatu umoja. Pia zipo kasida na nashidi zilizo weza kutumia nafsi ya tatu wingi. Mfano wa nashidi ilotumia nafsi ya tatu wingi ni nashidi ya “Palestina”;

__Wa__meunda system hawaendi mahakamani
__M__naua victims kwa helicopter angani
__M__naua wakulima wakati wako shambani
__M__naua kina mama kwa kivuli cha amani

Nashidi hii imetumia nafsi ya tatu wingi kwa kuwaelezea watu wengine neno "wameunda" linaonesha wazi matumizi ya nafsi ya tatu wingi. Mfano wa kasida ilotumia nafsi ya tatu wingi ni kasida ya ya "waliosema hayawi";

__Wa__lio sema hayawi ooh hayawi
Mbona leo yamekuwa ooh yamekuwa

Kasida hii imetumia nafsi ya tatu wingi kwa kutuia neno "waliosema". Matokeo haya yanathibitika kupitia msingi wa Nadharia ya Umuundo unaoeleza kuwa, tafauti za kazi moja ya fasihi na nyingine inatokana na namna kazi hizo zinavyotumia sifa na vipengele vya lugha na fasihi yenyewe. Hivyo, kutafautiana katika sifa hii, kunadhihirisha tafauti ya kasida na nashidi katika muktadha huu.

4.5 Matumizi ya Tamathali za Semi

[12] anaelezea kuwa tamathali za semi ni fungu la maneno lililogeuzwa maana yake kamili ili kuwakilisha maana nyingine. Kuna makundi matatu makuu ya tamathali za semi ambayo ni; tamathali za mafumbo, tamathali za mlinganisho na tamathali za msisitizo. Kasida na nashidi za Kiswahili hutumia tamathali za semi, watoa taarifa wameelezea kuwa tamathali za semi huchangia kupamba na kuleta mvuto kwa kasida na nashidi. [12] ameweza kuzichambuwa tamathali za semi kama ifiatavyo kwa kuonesha pia zilivyotumika kwenye kasida na nashidi za Kiswahili. Mfano wa kasida na nashidi zilizo tumia tamathali za semi za mafumbo. Aidha, matumizi ya tamathali za semi katika kasida na nashidi yanaweza kufafanuliwa vizuri kupitia Nadharia ya Umuundo ambayo hujikita katika kuchunguza namna vipengele vya lugha vinavyotumika katika kujenga maana, mtindo na athari za kisanaa katika kazi za fasihi. Kwa mujibu wa [2], Nadharia ya Umuundo huzingatia lugha kama mfumo maalumu wa alama zinazohusiana ili kutoa maana. Hivyo, matumizi ya tamathali za semi katika kasida na nashidi ni sehemu ya mfumo huo wa kiisimu unaobeba maudhui na kuongeza uzito wa ujumbe kwa hadhira.

4.5.1 Tafsida

[12] anaelezea kuwa tafsida ni maelezo yanayolenga kupunguza makali ya maneno. Hii ni tamathali ambayo inaonesha heshima kwa kutumia maneno ya kuficha matusi. Mfano katika nashidi ya "Ndoa"

Je masomo walikwambia mlango usiwe wazi
Sio kila ajae apite tu kizingiti kihifadhi

Nashidi hii imemuhisia mke kujihifadhi na kulinda amana ya mume wake kwakuto kumsaliti. Pia mfano wa kasida ya "Hongera Mwanangu";

Nami nitawatazama niwajuwe mwisho wao
Wamegeuka samaki walana wao kwa wao

Msanii ametumia tafsida kwa kupunguza ukali wa maneno kwa kuwasema watu ambao wanafanyiana fitina wao kwa wao. Kupitia Nadharia ya Umuundo, matumizi ya tafsida yanaonesha namna lugha inavyounda maana ya ndani kupitia uteuzi maalumu wa maneno. Kwa mujibu wa [4], uchaguzi wa maneno katika kazi ya fasihi una nafasi kubwa katika kujenga athari za kisanaa na kimawasiliano. Hivyo, matumizi ya tafsida katika kasida na nashidi yanaonesha mfanano wa kimtindo kutokana na watunzi wa tanzu hizi kutumia lugha ya upole na heshima ili kufikisha ujumbe kwa jamii bila kutumia maneno makali. Aidha, matumizi haya yanaonesha jinsi vipengele vya semantiki vinavyotumika kujenga maadili na kuhifadhi utamaduni wa jamii ya Waswahili wa Zanzibar.

4.5.2 Dhihaka

[12] anaelezea kuwa dhihaka ni maelezo yanayokusudia kubeza jambo na hulenga kudunisha au kudhalilisha. Katika kasida na nashidi tamathali hii yasemi hudhihirika. Mfano katika nashidi ya "Barua ya Mzee"

Mbele ya kadamnasi ulilia uombewe
Wee mzee hujatulia yakubidi upepewe
Kila mtu ataubeba mzigo wake mwenyewe

Nashidi hii inamdhihaki mzee ambae alifanya maamuzi yakufuata njia nzuri ya dini na baadae kugeuka ndipo msanii anaonesha kuwa mzee hajielewi kwa kurudi kulekule. Mfano wa kasida ya "Usiyajazi Masusu";

Unayajaza masusu, kwamambo yasokuhusu
Wewe mshamba ujuwe, na pia ni mwanagenzi

Kasida hii imeonesha zihaka kwa kumwita mshamba asiyejuwa kitu. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa kumekuwa na mfanano wa kimtindo baina ya nashidi na kasida. Hivyo ni wazi kuwa, nashidi zinafanana na kasida katika mtindo wa kutumia vipengele mbalimbali vya lugha katika fasihi ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Nadharia ya Umuundo, matumizi ya dhihaka yanaonesha namna vipengele vya lugha vinavyoweza kujenga maana fiche na athari za kihisia kwa hadhira. [7] anaeleza kuwa uchambuzi wa kiisimu katika fasihi huzingatia namna lugha inavyotumiwa kuwasilisha ujumbe wenye athari maalumu kwa jamii. Hivyo, matumizi ya dhihaka katika kasida na nashidi yanaonesha kuwa watunzi wa kazi hizi hutumia lugha kwa mtindo unaofanana ili kukosoa tabia zisizokubalika katika jamii kupitia kejeli na kubeza hali fulani.

4.5.3 Sitiari

[12] anaelezea kuwa sitiari ni maelezo yanayolinganishia na kuhusisha vitu vilivyo tafauti kitabia na kimaumbile. Maana na hisia ya kitu kimoja huhamishiwa kwenye kitu kingine. Mfano katika nashidi ya "Udhalilishaji";

…Dokta Mwinyi chuma...

Nashidi hii imeweza kulinganisha mtu na chuma bila kutumia kiunganishi chochote. Mfano wa kasida iliotumia sitiari ni kasida ya “Mama yangu”;

.. mama yangu nuru yangu…

Kasida hii imeweza kumfananisha binadamu na nuru bila kutumia kiunganishi chochote. Kasida hii imeonesha zihaka kwa kumwita mshamba asiyejuwa kitu. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa kumekuwa na mfanano wa kimtindo baina ya nashidi na kasida. Hivyo ni wazi kuwa, nashidi zinafanana na kasida katika mtindo wa kutumia vipengele mbalimbali vya lugha katika fasihi ya Kiswahili. Kupitia Nadharia ya Umuundo, matumizi ya sitiari yanaonesha jinsi lugha ya fasihi inavyounda maana kupitia uhusiano wa alama na ishara mbalimbali za kiisimu. [8] wanaeleza kuwa maana katika kazi ya fasihi hutokana na namna vipengele vya lugha vinavyohusiana katika muundo wa kazi husika. Hivyo, matumizi ya sitiari katika kasida na nashidi yanaonesha mfanano wa kimtindo kwa sababu watunzi wa kazi hizi hutumia uhamishaji wa maana kutoka kitu kimoja kwenda kingine ili kuimarisha ujumbe na kuongeza mvuto wa kisanaa.

4.5.4 Tashibihi

[12] anaelezea kuwa tashibihi ni maelezo ya mshabaha kwa madhumuni ya kulinganisha mambo, vitu au hali mbili. Mfano katiaka nashidi ya “Zawjat”;

…. Mimi ni mfano wa kizuri kitabu lakini wewe kwangu ni yamuhimu karatasi….

Nashidi hii imeweza kulinganisha binadamu pamoja na kitabu na ulinganisho huo umefanywa kwa kutumia kiunganishi. Mfano wa kasida ilio tumia tashibiha ni kasida ya “Mzuri kama ua”

Bibi harusi uyoo ni mzuri kama ua…

Kasida hii imeweza kutumia tamathali ya semi ya tashibihi kwa kumfananisha binadamu na ua lakini pia ulinganishi huu umetumia kiunganishi cha “kama”. Kasida hii imeonesha zihaka kwa kumwita mshamba asiyejuwa kitu. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa kumekuwa na mfanano wa kimtindo baina ya nashidi na kasida. Hivyo ni wazi kuwa, nashidi zinafanana na kasida katika mtindo wa kutumia vipengele mbalimbali vya lugha katika fasihi ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Nadharia ya Umuundo, matumizi ya tashibihi yanaonesha namna lugha ya kifasihi inavyojengwa kwa kutumia mahusiano ya vipengele vya kiisimu ili kuleta maana na mvuto wa kisanaa. [4] wanaeleza kuwa matumizi ya lugha ya kulinganisha huongeza nguvu ya mawasiliano katika kazi za fasihi. Hivyo, tashibihi zinazotumika katika kasida na nashidi zinadhihirisha namna watunzi wa kazi hizi wanavyotumia mfumo unaofanana wa lugha katika kuwasilisha hisia, mafunzo na maadili kwa hadhira yao.

4.5.5 Tashihisi

[12] anaelezea kuwa tashihisi ni maelezo ambayo hukipa kitu au mnyama sifa za binadamu. Kasida na nashidi huweza kutumia mbinu hii kuweza kuzipamba kazi zao. Mfano wa kasida ilotumia mbinu hii ni kasida ya “Kiama”

…. Mikono itaongea…

Kasida hii imeweza kuonesha hali ya siku ya kiama kuwa hata mikono itazungumza jambo ambalo sio kawaida. Mfano wa nashidi iliyotumia tashihisi ni nashidi ya “Unaweza”;

…. Muda utaongea….

Nashidi hii imeweza kutumia tashihisi kwakubebesha muda uwezo wa mwanadamu. Kasida hii imeonesha zihaka kwa kumwita mshamba asiyejuwa kitu. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa kumekuwa na mfanano wa kimtindo baina ya nashidi na kasida. Hivyo ni wazi kuwa, nashidi zinafanana na kasida katika mtindo wa kutumia vipengele mbalimbali vya lugha katika fasihi ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Nadharia ya Umuundo, tashihisi ni sehemu ya matumizi ya lugha yanayoonesha ubunifu wa kisanaa unaotokana na uhusiano wa vipengele vya lugha katika kazi ya fasihi. [2] anaeleza kuwa mtindo wa kazi ya fasihi hujengwa kupitia matumizi maalumu ya lugha yenye kuibua taswira na hisia kwa hadhira. Hivyo, matumizi ya tashihisi katika kasida na nashidi yanaonesha jinsi watunzi wa kazi hizi wanavyofanana katika kutumia lugha ya picha ili kuongeza mvuto, kusisitiza ujumbe na kuifanya hadhira iweze kutafakari kwa kina maana iliyokusudiwa.

4.5.6 Mubaalagha

[12] anaelezea kuwa mubalaalagha ni kutia chuku au chumvi katika maelezo. Kasida na nashidi za Kiswahili hutumia tamathali hii ya mubaalagha. Mfano wa nashidi iliyotumia tamathali hii ni nashidi ya “Hazina Yetu”;

Nashidi hii imetumia mubaalagha kwa kuonesha Kiswahili kinamabawa na kinapepea dunia nzima, jambo ambalo ni kutia chumvi kwasababu Kiswahili kinatumika nchi nyingi duniani lakini sio dunia nzima. Mfano wa kasida inayotumia tamathali hii ni kasida ya “Mtume wetu Hashimu”;

Utadhani kajiumba namna alivyo pabwa
Si mnene si mwembamba kakamilika nabia

Nashidi hii imetumia mubaalagha kwa kusema mtume amepambika kama amejiumba mwenyewe jambo ambalo haliwezekani mtu kujiumba mwenyewe. Matokeo haya yanathibitika kupitia msingi wa Nadharia ya Umuundo unaoeleza kuwa, tafauti za kazi moja ya fasihi na nyingine inatokana na namna kazi hizo zinavyotumia sifa na vipengele vya lugha na fasihi yenyewe. Hivyo, kutafautiana katika sifa hii, kunadhihirisha tafauti ya kasida na nashidi katika muktadha huu.

4.6 Matumizi ya Methali

[2] anaongeza kuwa methali ni kauli fupifupi zenye dhima ya kutoa fundisho, kuonya au kuhimiza tabia njema katika jamii. Katika jamii ya Wazanzibar methali hutumika kufundisha maadili na kuelezea falsafa za maisha. Wasanii wa kasida na nashidi huweza kutumia methali katika kazi zao, watoa taarifa wameelezea kuwa kasida na nashidi za Kiswahili hutumia methali kwa kuzipamba kazi na kufikisha ujumbe katika jamii. Mfano wa nashidi ambayo imetumia methali ni nashidi ya “Kiswahili”

Asie na mwana abebejiwe

Nashidi hii imetumia methali hii kwa kuonesha Waswahili kuwa kama hatuna lugha yetu wenyewe basi tuzidi kuzipa kipaumbele lugha za wengine. Mfano wa kasida iliyotumia methali ni kasida ya "Asomtu ana Mungu"

…..Asomtu ana Mungu ana Mungu……

Matumizi ya methali katika kasida na nashidi yanaweza kufafanuliwa vizuri kupitia Nadharia ya Umuundo ambayo hujikita katika kuchunguza namna vipengele vya lugha vinavyotumika kujenga maana katika kazi za fasihi. Kwa mujibu wa [7], vipengele vya kiisimu kama vile semantiki na sintaksia vina nafasi kubwa katika kujenga mtindo wa kazi ya fasihi. Hivyo, matumizi ya methali katika kasida na nashidi yanaonesha namna watunzi wa kazi hizi wanavyotumia lugha ya kifasihi yenye hekima na mafumbo ili kuwasilisha mafunzo kwa jamii. Aidha, methali hizi hujenga mfanano wa kimtindo baina ya kasida na nashidi kwa sababu tanzu hizi zote hutegemea matumizi ya lugha ya mkato yenye maana pana katika kufikisha ujumbe kwa hadhira.

Kwa mujibu wa [8], Nadharia ya Umuundo hueleza kuwa maana ya kazi ya fasihi hutokana na mahusiano ya vipengele mbalimbali vya lugha vinavyounda kazi husika. Kwa msingi huo, matumizi ya methali katika kasida na nashidi yanaonesha jinsi vipengele vya lugha vinavyohusiana katika kujenga maadili, falsafa na ujumbe wa kijamii. Hivyo, mfanano huu wa matumizi ya methali unadhihirisha kuwa kasida na nashidi zina uhusiano mkubwa wa kimtindo katika fasihi ya Kiswahili ya Zanzibar.

4.7 Matumizi ya Mafumbo

[1] anaelezea kuwa mafumbo ni usemi wa kisanaa unaoficha maana halisi ili wasikilizaji watumie akili na maarifa yao kuufumbua. Mafumbo husaidia sana kuipamba kazi ya sanaa na kuonesha ubora au ubobevu wa msanii, katika kasida na nashidi za Kiswahili huweza kutumia mafumbo ili kuweza kufikisha ujumbe sehemu waliyo ikusudia. Watoa taarifa wameelezea kuwa kasida na nashidi hutumia mafumbo kwa kuongeza ladha katika tungo na kuonesha utafauti. Kuna baadhi ya kasida na nashidi zinazosomwa Zanzibar hutumia mafumbo. Mfano wa nashidi ya "Kiswahili"

Asie na mwana abebejiwe
Napata utata ni kipi nikielewe
Kwamba hatuna mwana ndomana tunabeba mawe
Au huyo mwana sio wakwetu wenyewe

Nashidi hii imetumia fumbo kwa kuwauliza Waswahili kwanini wanatumia lugha za kigeni maofisini na sehemu mbalimbali katika jamii au hatuna lugha yetu wenyewe. Mfano wa kasida ya "vigelegele";

Kuwa na maneno laini, yatowa nyoka pangoni
Kwa penzi ni fasheni, mume atabaki ndani

Kasida hii imetumia mafumbo kufikisha ujumbe kwa biharusi kwa kumuhasasa azungumze maneno laini ili aweze kumtuliza mumewe na kumfanya abaki ndani. Matumizi haya ya mafumbo yameweza kuonesha upekee wa waandishi na mvuto wa lugha. Matokeo haya yanathibitika kupitia msingi wa Nadharia ya Umuundo unaoeleza kuwa, tafauti za kazi moja ya fasihi na nyingine

inatokana na namna kazi hizo zinavyotumia sifa na vipengele vya lugha na fasihi yenyewe. Hivyo, kutafautiana katika sifa hii, kunadhihirisha tafauti ya kasida na nashidi katika muktadha huu.

4.8 Matumizi ya Methali

[2] anaongeza kuwa methali ni kauli fupifupi zenye dhima ya kutoa fundisho, kuonya au kuhimiza tabia njema katika jamii. Katika jamii ya Wazanzibar methali hutumika kufundisha maadili na kuelezea falsafa za maisha. Wasanii wa kasida na nashidi huweza kutumia methali katika kazi zao, watoa taarifa wameelezea kuwa kasida na nashidi za Kiswahili hutumia methali kwa kuzipamba kazi na kufikisha ujumbe katika jamii. Mfano wa nashidi ambayo imetumia methali ni nashidi ya "Kiswahili":

Asie na mwana abebejiwe

Nashidi hii imetumia methali hii kwa kuonesha Waswahili kuwa kama hatuna lugha yetu wenyewe basi tuzidi kuzipa kipaumbele lugha za wengine. Mfano wa kasida iliyotumia methali ni kasida ya "Asomtu ana Mungu":

…..Asomtu ana Mungu ana Mungu……

Kupitia Nadharia ya Umuundo, matumizi ya methali katika kasida na nashidi yanaweza kufafanuliwa kwa kuzingatia namna vipengele vya lugha vinavyojenga maana na kuimarisha mtindo wa kazi za fasihi. Kwa mujibu wa nadharia hii, methali ni sehemu ya miundo ya lugha inayobeba maana za kijamii na kisanaa ndani ya kazi ya fasihi. Hivyo basi, matumizi ya methali katika kasida na nashidi yanaonesha namna wasanii wanavyotumia miundo ya lugha ya jadi katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yao. Aidha, Nadharia ya Umuundo inaeleza kuwa maana ya kazi ya fasihi hutokana na uhusiano wa vipengele vya lugha vilivyomo ndani ya kazi hiyo. Katika mifano hii, methali zimeweza kujenga athari ya kisemantiki na kimtindo kwa kuwasilisha maadili, maonyo na mafundisho ya jamii ya Waswahili kwa lugha yenye ufupi lakini yenye maana pana.

Vilevile, nadharia hii imesaidia kubainisha kuwa kasida na nashidi zinafanana katika matumizi ya methali kama kipengele cha lugha kinachojenga mfanano wa kimtindo baina ya tanzu hizi mbili. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa kumekuwa na mfanano wa kimtindo baina ya nashidi na kasida. Hivyo ni wazi kuwa, nashidi zinafanana na kasida katika mtindo wa kutumia vipengele mbalimbali vya lugha katika fasihi ya Kiswahili.

4.9 Matumizi ya Misemo

[11], msemo ni kauli maarufu inayotumika kuashiria jambo fulani kwa njia ya mafumbo au picha, lakini si lazima iwe na maana kamili kama methali. Katika jamii ya Wazanzibari misemo ni sehemu muhimu ya mawasiliano ya kila siku misemo huonesha ujuzi na hekima alizonazo mtu, hata wasanii wa kasida na nashidi za Kiswahili huweza kutumia misemo kwenye kazi zao kwa kuonesha uhodari wao wa utunzi, watoa taarifa wameelezea kuwa kasida na nashidi za Kiswahili hutumia misemo kwa kuzifanya kazi zao ziwe bora na kuwavutia wasikilizaji pia misemo hutowa ujumbe katika kazi zao. Hivyo basi misemo inamchango mkubwa katika fani ya sanaa ya kasida na nashidi za Kiswahili kwakuzifanya ziwe bora na mvuto wa kipekee. Mfano wa nashidi iliyotumia msemo ni nashidi iitwayo "Baba";

…Eeh mwenda mbio mwache haende weee riziki haiwaniwa
Mungu akitaka kupa hakuletei barua
hukupa usingizini pasi na mtu kujuwa

Nashidi hii imeelezea kuwa riziki haipupiwi kila mtu Mwenyezi Mungu kamuandikia riziki yake. Mfano wa kasida iliyotumia misemo ni kasida ya "Hongera Mwanangu";

…. wajane wapaliliwa kama mpunga shambani….

Msemo huu unamuhasa biharusi atulie kwenye ndoa yake kila siku wajane wanazidi kuongezeka kuwa wengi. Misemo imeweza kuzipamba kazi hizi nakuonesha kuwa zina ladha halisi ya Waswahili. Kupitia nadharia ya fasihi linganishi katika msingi wake mdogo wa mtindo umeweza kusaidia kuchambuwa na kubainisha mtindo wa matumizi ya misemo iliyotumika kwenye kasida na nashidi za Kiswahili. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa kumekuwa na mfanano wa kimtindo baina ya nashidi na kasida. Hivyo ni wazi kuwa, nashidi zinafanana na kasida katika mtindo wa kutumia vipengele mbalimbali vya lugha katika fasihi ya Kiswahili.

Aidha, matumizi ya misemo katika kasida na nashidi yanaweza kueleweka vizuri kupitia Nadharia ya Umuundo ambayo huchunguza namna lugha inavyotumika kujenga maana katika kazi za fasihi. Kwa mujibu wa [2], mtindo wa kazi ya fasihi hujitokeza kupitia uchaguzi wa maneno, mpangilio wa sentensi pamoja na matumizi ya lugha ya picha. Hivyo, matumizi ya misemo katika kasida na nashidi yanaonesha namna watunzi wa kazi hizi wanavyotumia lugha ya mafumbo na picha ili kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kisanaa.

[4] wanaeleza kuwa matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi huweza kuibua athari maalumu kwa hadhira kutokana na namna vipengele vya kiisimu vinavyopangwa. Kwa msingi huo, matumizi ya misemo katika kasida na nashidi yanaonesha mfanano wa kimtindo kwa sababu watunzi wa kazi hizi hutumia misemo kama sehemu ya kuimarisha mawasiliano, kuongeza mvuto wa lugha na kuonesha utamaduni wa jamii ya Waswahili. Aidha, matumizi ya misemo yanaonesha jinsi vipengele vya semantiki na sintaksia vinavyotumika katika kujenga ubunifu wa kisanaa ndani ya kasida na nashidi za Kiswahili Zanzibar.

5.0 Hitimisho

Utafiti huu umebainisha kuwa kasida na nashidi za Kiswahili katika jamii ya Zanzibar zinafanana kwa kiasi kikubwa katika mtindo wa matumizi ya lugha na mbinu za kisanaa. Mfanano huo unajitokeza kupitia vipengele mbalimbali kama vile takriri, lugha ya kishairi, tamathali za semi, mafumbo, methali na misemo, ambavyo kwa pamoja hujenga mvuto wa kisanaa, kusisitiza ujumbe, na kurahisisha upokeaji wa maudhui kwa hadhira. Vipengele hivi pia vinaonesha kuwa tanzu zote mbili zinategemea sana ubunifu wa lugha katika kuwasilisha maadili, mafundisho ya dini na ujumbe wa kijamii.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Umuundo, imebainika kuwa mfanano huu unatokana na namna vipengele vya lugha vinavyopangwa, kuhusiana na kuunda mfumo wa maana ndani ya kazi za fasihi. Hii ina maana kwamba, licha ya tofauti za majina na mazingira ya uwasilishaji, kasida na

nashidi zinashirikiana katika misingi ya kimuundo wa lugha unaozifanya ziwe na mtindo unaokaribiana sana. Hivyo, tanzu hizi zinaweza kuonekana kama sehemu ya mfumo mmoja wa kifasihi unaoendeleza urithi wa lugha na utamaduni wa Waswahili wa Zanzibar.

Kutokana na matokeo haya, inapendekezwa kuwa tafiti zaidi zifanywe kuchunguza kwa upana uhusiano wa tanzu nyingine za fasihi simulizi na andishi ili kubainisha zaidi mwingiliano wa kimtindo na kiisimu. Aidha, inashauriwa kuwa kasida na nashidi ziendelee kuhifadhiwa, kuandikwa na kuchambuliwa kitaaluma ili kuimarisha urithi wa fasihi ya Kiswahili na kuongeza matumizi yake katika elimu na jamii kwa ujumla.

Marejeo

[1] Mulokozi, M. M. (1996). Fasihi ya Kiswahili. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
[2] Wamitila, K. W. (2003). Kamusi ya fasihi: Istilahi na nadharia. Nairobi: Focus Books.
[3] Finnegan, R. (1970). Oral literature in Africa. Oxford: Oxford University Press.
[4] Leech, G., & Short, M. (1981). Style in fiction. London: Longman.
[5] Kothari, C. R. (2014). Research methodology: Methods and techniques. New Delhi: New Age International Publishers.
[6] Ponera, A. (2019). Misingi ya utafiti wa kitaamuli na uandishi wa tasnifu. Dar es Salaam: Central Tanganyika Press.
[7] Jilala, H. (2016). Misingi ya fasihi linganishi: Nadharia, mbinu na matumizi. Dar es Salaam: Daudi Publishing Company.
[8] Wafula, R. M., & Njogu, K. (2007). Theory of literary criticism. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
[9] Senkoro, F. E. M. K. (1988). Ushairi: Nadharia na tahakiki. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
[10] Kezilahabi, E. (1976). Ushairi wa Kiswahili. Dar es Salaam University Press.
[11] Kezilahabi, E. (1985). Kazi za fasihi na lugha. Dar es Salaam University Press.
[12] Madumulla, J. S. (2022). Nadharia ya fasihi na uhakiki wake. Dar es Salaam University Press.
[13] TUKI. (2014). Kamusi ya Kiswahili sanifu. Dar es Salaam: TUKI : Taasis ya Uchunguzi wa Kiswahili.